KUHUBIRI / PREACHING

Kuhubiri ni kutangaza neno la Mungu kwa wanadamu na wale ambao wameitwa na Mungu kufanya hivyo. Hii ndio njia ambayo Mungu anaitumia kuzungumza neno Lake kwa watu. Mahubiri ya kweli yanafaa sana kwa kanisa ambalo linaendelea vyema kiroho. Ikiwa kanisa halitazingatia kuhubiri ukweli wa neno la Mungu, kanisa hilo litakuwa dhaifu kiroho na halitaweza kufanikiwa katika kazi ya Mungu.

I. **Je, kuhubiri ni kufanya nini?**

1. Agano Jipya linataja neno mahubiri zaid ya mara 60. Kuna maneno manne tofauti amabyo Agano Jipya linatumia kuhusu kuhubiri.

A. Kerusso ni neno ambalo linamaanisha kutangaza ujumbe wa mfalme. Hii inamaanisha kwamba mhubiri huwa hazungumzi maneno yake, bali yeye huzungumza kwa mamlaka maneno ya mfalme. Mhubiri ni lazima afahamu kwamba yeye ameitwa na Mungu na kwa sababu hiyo, yeye ana mamlaka kutoka kwa Mungu.

B. Evangelizo ni neno ambalo linamaanisha kueneza habari njema. Malaika katika Luka 2:10 alieneza habari njema. Hii inamaanisha kuhubiri injili.

i. Mara kwa mara maneno haya mawili, kerusso na evangelizo yana maana ya kutangaza habari njema. Luka 4:18-19, “Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa sababu amenitia mafuta kuwaletea (evangelizo) maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia (Keresso) wafungwa kuifunguliwa kwao na vipofu kupata kuona tena, kuwaweka huru wanaoonewa na kutangaza (Kerusso) mwaka wa Bwana uliokubalika.

C. Martureo - neno hili linamaanisha kuhushudia. Mhubiri huwa anatangaza ukweli wa Biblia.

D. Didasko - neno hili linamaanisha kueleza katika maneno ambayo inafahamika ujumbe wa injili unamaanisha nini kwa wale ambao wanausikiliza. Kwa ufupi ni kwamba mhubiri anapaswa kueleza kile ambacho Biblia inamaanisha na jinsi msikilizaji anapaswa kuishi maisha yake kulingana na ujumbe wa Biblia.

2. Mhubiri anapokuwa anahubiri, huwa anatumia maneno haya katika ujumbe wake. Kwa mfano katika Matendo ya Mitume 15:35, tunasoma kwamba Paulo na baranaba walimaliza muda wakifundisha na kuhubiri neno la Mungu. Mfano mwingine wa mhubiri kutumia maneno haya ni Matendo ya Mitume 28:31. Hapa tunaona kwamba Paulo alitumia nyumbani mwake kama mahali pa kuhubiri na kufundisha (Kerussa na didasko).

A. Kuhubiri ni Kufundisha.

II. Je, mahubiri mazuri ya Biblia ni mahubiri ya aina gani?

1. Hii inamaanisha kueleza maana halisi ya kifungu ambacho kinazungumziwa. Mhubiri anapaswa kueleza kwa uaminifu kile ambacho Biblia inasema. Mwandishi wa Biblia alikusudia maana moja alipokuwa anaandika. Kwa sababu hii mhubiri anapswa kuzingatia maana hii ya mwandishi. Ni jambo la muhimu sana kuona kwamba mhubiri anasema kile ambacho Biblia inasema na wala si maneno yake matupu.

A. Maombi ni ya muhimu sana katika mahubiri. Wakati ambao unamaliza katika maombi na wakati ambao unamaliza katika kutayarisha mahubiri ni wakati wa muhimu sana.

B. Wakati ambao unamaliza katika kutayarisha mahubiri na kuomba ni wakati mzuri sana Zaidi kuliko wakati unamaliza ukihubiri.

i. Mungu anataka kila muhubiri aliheshimu neno lake. Mungu anataka kila mhubiri aliamini neno lake. Mhubiri anapaswa kukumbuka kwamba kile ambacho Biblia inamaanisha ndio kile ambacho Mungu anamaanisha.

ii. Tunapaswa kujifunza kila neno la Biblia na kukubali maana yake.

iii. Tunapaswa kufahamu history ya kile ambacho unakisoma.

iv. Ni lazima tufahamu mazingira ambamo Biblia iliandikwa ndani yake. Mfano ni kuhubiri 1 Wakorintho 2:6-11. Kuna wahubiri wengi ambao huwa wanazungumza kuhusu mbinguni katika kifungu hiki. Huu si ukweli kwa sababu mbinguni haitajwi hapa katika kifungu hiki. Kifungu hiki kinafundisha kwamba watu wa Mungu wanaweza kuona na kufahamu mambo ya kiroho ambayo imefichika kutoka kwa wale ambao hawajaokoka.

v. Ni lazima tufahamu historia ya mazingira ambao kifungu kiliandikwa ndani mwake. Mfano ni katika Matendo ya Mitume 19:1-2 wakati Paulo alipowauliza watu ambao walikuwa wa dini kama walikuwa wamempokea Roho Mtakatifu walipoaamini. Walisema hapa. Jambo hili halikukubalika katika nyakati za Abrahamu. Matendo ya Mitume 19, ni baada ya Pentekote baada ya kanisa kupewa Roho Mtakatifu. Jibu la hap aka watu wale lilikuwa kwa sababu wao walikuwa hawajaokoka. Paulo alizungumza nao kama watu ambao hawajaokoka jambo ambalo liliwafanya sasa kufahamu hali yao na kuokoka.

vi. Je, vifungu vingine vya Biblia vinasema nini kuhusu kifungu hiki? Kukumbuka kwamba ni lazima uyatumie maandiko kufafanua maandiko. Kwa mfano, hufai kuhubiri kuhusu Melkizedeki ukitumia Mwanzo 14:18-24. Unahitaji pia Waebrania 5:5-10 na 7:1-28.

vii. Je, kifungu hiki kinaeleza aje kumhusu Kristo? Kukumbuka kwamba Biblia yote inazungumza kumhusu Kristo pekee. Wakati mwingine ni vigumu kuona Kristo, lakini ni lazima tuwe waangalifu sana. Kwa mfano kitabu cha Mhubiri kina maswali ambayo yanatufanya tumtamani Mungu.

viii. Je tunawezaje kufafanua Biblia kwa njia ya uaminifu? Je, tunawezaje kueleza kwa uaminifu yale ambayo yaliyomo katika Biblia? Tunaweza kuyfanya hivi kwa kuisoma na kujifunza Biblia na kuomba Mungu atusaidie kufahamu neno Lake.

2. Kufundisha ukweli wa Biblia ni jambo la muhimu sana.

A. Mahubiri yanapaswa kujawa na mafundisho mengi sana. Kwa kusema hivi tunamaanisha kwamba tunapaswa kufundisha mambo kama kuumbwa kwa kila kitu, wokovu, hukumu, mbinguni, jahanum na mambo mengi ya Biblia.

B. Mahubiri yetu yanapaswa kusudia kuwasaidia wengi kuelewa ukweli wa Biblia (Warumi 6:17).

C. Je, ni nini ambacho kinafanyika wakati Biblia haihubiriwi vyemka kabisa.

i. Watu hawamwabudu Mungu jinsi ipasavyo kwa sababu wao hawaelewi Mungu ni nani. Hii inatokana na ukosefu wa mafundisho mazuri. Wao hawafahamu Mungu mkuu ambaye anatawala na ni mwenye upendo mkuu.

ii. Watu wengi hawaelewi uhusiano mwema ambao wale wameokoka wanao pamoja na Mungu.

iii. Wengi ambao wameokoka, hawaelewi Baraka zao kwa sababu ya ukosefu wa mafundisho mazuri.

a. Wengi wanasahau bara ambazo wanazo kwa sababu ya kusamehewa dhambi na kuhakikishiwa mbinguni.

b. Wengi hawafahamu kwamba wao wamefanywa kuwa wana wa Mungu na kwa sababu hiyo hali yao mbele ya Mungu ni tofauti kabisa.

c. Wengi hawafurahia Baraka za kuishi maisha yao kabisa wakiwa wana wa Mungu. Kizazi cha wakristo wengi ni bora sana kuliko kizazi cha wale ambao hawajaokoka.

iv. Wengi ambao wameokoka, hawajui jinsi wanapaswa kuishi maisha yao. Tunapaswa kumtii Mungu na kufanya hivi, tunapaswa kumjua Mungu ni nani. Ni kazi ya muhubiri kuwafunza watu neno la Mungu.

v. Kwa sababu ya wengi kukosa kufahamu Mungu, wao hawawezi kumshuhudia Kristo. Wahubiri wanapswa kuwafunza wasikilizaji wao jinsi ya kumshuhudia Kristo.

vi. Wengi hawajui kuishi maisha matakatifu inamaanisha nini.

vii. Wengi hawajui kuomba iwapasavyo.

3. Mahubiri yanapaswa kuwa mpangilio mwema kabisa. Mahubiri yanapaswa kuwa na umoja na ujumbe ambao msingi wake ni Kristo. Mahubiri yanapaswa kuwa na mpangilio ambapo yanaambatana na maana ni moja. Ni lazima mahubiri yapangwe vyema kabisa.

A. Utangulizi. Hii ni sehemu ambayo inawaelezea watu kuhusu yale ambayo unaenda kuyazungumzia. Hii inakuzaidia kuwafanya watu wawe na tamaa yay ale ambayo unaenda kuyazunguzia. Hii sehemu haswa inafanywa kwa kueleza hadithi.

i. Utangulizi haufai kuwa mrefu sana. Ni utangulizi na wala si mahubiri yenyewe.

B. Majadiliano: Baada ya utangulizi ni wakati wa kueleza ukweli wa neno la Mungfu ambalo umeliandaa.

i. Ni lazima uwe na kusudi. Ni lazima wasikilizaji wako waone kwamba kuna mahali ambapo unaelekea katika mahubiri yako. Ni lazima kusudi lako lazima liwe rahisi la kueleweka nma kila mtu. Hili ndilo kusudi lako katika mahubiri yako kwamba kila mtu aelewe kile ambacho unahubiri.

ii. Hakikisha kwamba mahubiri yako si marefu sana ambayo itawafanya wasikilizaji wako waanze kulala. Pia hakikisha kwamba unahubiri kuhusu jambo au kifungu klwa muda kuwawezesh wale ambao wana sikiliza kufahamu vyema.

iii. Hakikisha kwamba humalizi muda mrefu kwa jambo moja. Hakikisha kwamba kila sehemu ya mahubiri yako unaipea muda sawa.

iv. Hakikisha kwamba katika mahubiri yako unawashawishi wasikilizaji wako kwa njia mzuri. Kwa mfano katika Mathayo 6:1-18, Bwana Yesu ataufundisha kuhusu matendo mazuri, maombi na kufunga. Kwanza Yesu anafundisha kile ambacho hatufai kufanya halafu anafundisha kuhusu kile ambacho tunapaswa kufanya. Fundisha kwamba yale ambayo hatufai kufanya, ndipo uyafundishe yale ambayo tunapaswa kuyafanya.

v. Tumia maneo mepesi ili kuwafanya wasikilizaji wako wawe makini.

C. Muhtasari.

i. Muhtasari wako unapaswa kuzingatia yale ambayo umeyafundisha katika mahubiri yako.

ii. Muhtasari mwema unapaswa kuwa mfupi sana na wa kuwapa wasikilizaji changamoto na kuwakumbusha kuhusu yale ambayo umeyahubiri. Mara kwa mara ni kwamba mhutasari mzuri ndio utakumbukwa sana na wasikilizaji wengi.

iii.Ni vyema sana kuandika yale ambayo unataka wasikilizaji wako wayasikie na kuyakumbuka.

4. Hadi sasa, ni wazi kwamba kuhubiri ni jambo ambalo linahitaji kazi nyingi sana.

A. Mifano itasaidia sana katika kuwafanya wasikilizaji wako waelewe vyema sana. Mifano inawafanya wasikilizaji waone maneno yako katika mambo ambayo wanayaelewa sana.

i. Mara kwa mara huwa tunatengeneza mifano katika mawazo yetu kutokana na maneno ambayo tunayasikia kwa redia kuhus hadithi fulani.

B. Mifano ni nzuri sana kwa sababu inasaidia katika kufahamu ukweli. Mathayo 13 imejawa na mifano kwa mfano katika mistari ya 23,31,33,44,45 na 47. Mtume Paulo anatumia mifano katika Warumi 6 and 7 wakati anaposema kwamba wakristo hatufai kuishi katika dhambi kwa sababu sisi si watumwa tena wa dhambi. Anatumia mfano wa soko la watumwa ambapo ni rahisi kufahamu mtumwa fualni ni wa nani. Sisi ambao tumeokoka, tunapaswa kuishi kwa njia ambayo inaonyesha kwamba sisi ni watumwa wa Kristo, Yeye ndiye Bwana wetu.

C. Mifano huwa inafanya mahubir yetu yawasaide sana wale ambao wanayasikilzia. Baada ya kumsikiliza mnenaji kwa muda, mara watu huwa wanachoka na kuanza kuwaza mambo mengine. Ikiwa katikati mwa mahubiri yako unatumia mfano fulani, utawafanya watu wamakinike.

D. Mifano huwa inawasaid watu kukumbuka mambo muhimu katika mahubiri. Ikiwa utamsaidia mtu kuyatumia maneno yako katika mfano, utakuwa umemsaidia sana. Kwa mfano Luka 15 ambapo tunajifunza kuhusu mwana mpotevu ambayo ilijirudia na kuona kwamba anahiytaji kurudi kwa babake. Mstari wa 23, tunasoma kwamba baba alifurahi sana kuona kwamba mtoto wake amerudi na kwa sababu hii, aliandaa sherehe. Katika haya wasaidia watu kwa mfano. Unaweza kufanya hivi kwa kutoa mifano kwa kuwaeleza watu kuhsuhu sherehe ambazo wao huhudhuria kama harusi. Mifano kama hii inaweza kuwasaidia watu kukumbuka yale ambayo umeyafundisha kama kwamba Yesu hufurahia sana wakati mwenye dhambi anatubu.

5. Ni lazima mahubir yako kusudi lake liwe kuzungumza na wale ambao wanakusikiliza. Ni lazima ulishi mahitaji yao ya kiroho na ili waweze kutumia mahubiri hayo katika maisha yao ya kila siku. Hakikisha kwamba mahubiri yako ni mepesi kufahamu.

A. Sehemu moja ya mahubiri yako ni kuwaonyesha wasikilizija wako jinsi wanapaswa kuishi maisha yao kulingana nay ale ambayo umewafundisha.

B. Ni lazima kuwaonyesha watu jninsi ya kuishi maisha yao kulingana na mahubiri yako la sivyo mahubiri yako hayatakuwa yamekamilisha kusudi lake. Kukumbuka kwamba unapaswa kuwa unahubiri na kufundishi na wala si kuonyesha jinsi unajua sana.

i. Mfano wa kuihsi jinsi Biblia inafundisha ni Mwanzo 12:L1-9. Mhubiri anapaswa kuonyesha ni nini ambacho kinafanyika wakati Mungu anamwambia Abramu anondoka na kumwahidi. Mhubrir anaweza kuonyesha kwamba hii ni hadithi ambayo inahusu Imani ana utiifu. Jinsi ya kuishi kulingana mafundisho haya ni kuwaeleza wasikilizaji wake kwamba wanapaswa kuihsi maisha ya Imani na utiifu kwa Mungu.

C. Je, tunahakikishaje kwamba mafundisho yetu inazingatia jinsi ya watu kuishi maisha yao?

i. Hakikisha kwamba watu wanafahamu jinsi wanapswa kuishi kulingana na neno la Mungu. Mfano upo katika 19:21 wakati Yesu anamwambia kijana tajiri kile ambacho alifaa kukifanya.

ii. Kumbuka kwamba kuwaeleza watu kile ambacho wanafaa kukifanya na jinsi wanafaa kukifanya na ni kwa nini wanapaswa kukifanya. Mhubiri wa kweli ni lazima awe na upendo juu ya watu ambao anawahubiria. Unapaokuwa kuwa unawaeleza watu jinsi wanapaswa kuishi maisha yao na kuwahimiza waokoke. Fanya hivi kwa njia mzuri nay a heshima.

D. Kuhubiri ambako kunafaa ni wakati ambapo wale ambao unawahubiria unapoawaona wakijitahidi katika maisha yao kuishi kulingana na neno ambalo unawahubiria.

6. Ili uweze kuwafaidi wale ambao unawahubiria, ni vyema sana kujiandaa na kuandaa mahubiri yake vizuri sana. Kwa hivyo ni lazima uhakikishe kwamba unajianda vyema na pia unahubiri kwa njia ambayo itawafaidi wasikilizaji wako.

A. Hali ya moyo wako ni ya muhimu sana wakati unapokuwa unahubiri.

i. Mhubiri anapaswa kuwa mtu mwenye ujasiri. Ni lazima ahubiri ujumbe wa injili kwa ujasiri sana na asijali kama wengi wataukataa kwa sababu ni ujumbe wa Biblia. Kile kila mhubiri anapaswa kuelewa ni kwamba kazi yake ni kuwa mwaminifu kwa Mungu. Wewe usihubri ili uwapendeze watu.

ii. Mhubiri anapaswa kuwa wanyenyekevu tukikumbuka kwamba sisi ni wenye dhambi na nguvu zetu zinatoka kwa Mungu pekee.

iii. Mhubiri anapaswa kuwa mtu wa kweli. Ujumbe wako unapaswa kuwa wa kweli. Ni lazima uamini kile ambacho unahubiri.

iv. Mhubiri anapaswa kuelewa kile ambacho anakizungumzia.

v. Mhubiri anapaswa kuwa mtu mwenye heshima hata wakati anahubiri ujumbe mgumu sana.

vi. Mhubiri anapaswa kutumia mifano ambayo ianaeleweka ili aweze kueleweka.

B. Mhubiri lazima awe mwangalifu kuhusu yaled maneno ambayo anayatumia.

i. Lugha ambayo tunaitumia lazima iwe lugha nyepesi ya kueleweka.

a. Eleza jambo kwa sentesi

b. Hakikisha kwamba sentensi zako ni mfupi.

c. Tumia maneno mafupi ambayo yanaeleweka kabisa.

d. Tumia maneo ambayo wasikilizaji wako wanayaelewa. Pia hakikisha kwamba unafafanua maneo ambayo huenda wengine wako kuyaelewa.
i. Hakikisha kwamba unatumia njia mwafaka ya kujieleza katika lugha ambayo unatumia.

ii. Hakikisha kwamba unayatumia mamneno ambayo yataeleza wazi jambo ambalo unataka wasikilizaji wako walifahamu.

C. Sauti yako: hakiksiha kwamba unazungumza kwa sauti yako ya kawadia. Mara kwa mara unaweza kubadilisha jinsi unavyozungumza, polepole ai kwa sauti ya juu. Au pia unaweza kunyamaza kidogo kuwapa wasikilizaji wako na nafasi ya kufikiria.

D. Hakikisha kwamba pia unatumia ishara. Huwa tunafanya hivi kwa jinsi tunavyozungumza, tunavyowatazama wale ambao wanatusikiliza, au jinsi tunavyosimama au kuketi au kwa kutumia mikono yetu.

i. Hakikisha kwamza unawatazama watu kwa uso. Usiwe utazama tu njia katika madilisha. Hakikisha kwamba unawaonyesha kwamba unazungumza nao.

E. Jinsi unavyoonekana: Unapaswa kuvaa kwa njia ambayo inaonyesha heshima kwa wale ambao wanakusikilzia na kwa Mungu. Pia hakikisha kwamba usivaa kwa njia ambayo itafanya watu wawaze tu juu ya mavazi yako na wale si kuwa makini kwa neno la Mungu.

F. hakikisha kwamba usizungumza kwa muda mrefu hadi watu wachoke na kukusikilzia. Hakikisha kwamba unazungumza neno la Mungu pekee. Hakikisha unazingatia muda wako wa kuhubiri.

7. Hakikisha unazungumza kwa mamlaka, kwa furaha na kuwa upendo juu ya kile ambacho unazungumza kuhusu.

A. Ikiwa lengo ni kuona kwamba neno la Mungu linafanya kazi katika maisha ya wale ambao unawazungumzia, basi kumbuka kwamba unamhitaji Roho Mtaklatifu afanye kazi hii, kwa sababu ni nguvu zake ambao zinafanya kazi katika maisha ya watu (1 Wathesalonike 1:5).

B. Unapaswa kuwa na imani kwamba ujumbe wako ni wa muhimu sana kwa hivyo unapaswa kuueleza (2 Wakorintho 4:13). Kuna wengi ambao wanakufa bila Kristo, na kwa hivyo wanahitaji kusikia kumhusu Yesu kabla wafe. Unapaswa kuwa na Imani kubwa katika ujumbe ambao unahubiri, kiwango kwamba huwezi kuendelea bila kuueleza.

C. Unapaswa kueleza ujumbe wako kwa machozi mengi sana, kwa sababu huu ni ujumbe ambao unaleta uzima wa milele.

III. Kuhusu kuandaa mahubiri.

1. Usiongoje hadi huna muda wa kutosha wa kujiandaa vyema. Ikiwa wewe ni mtu ambaye anahubiri kila jumapili, basi unapaswa kuandaa ujumbe wako miezi au wiki kadhaa.

A. Hapa kuna hatua kadhaa kwa kadhaa ambazo unaweza kuzifuata.

i. Maliza muda kwa kuwaza na kuomba ili Mungu akuongoze katika maandalizi yake. Ikiwa unataka kuhubiri ujumbe ambao utazaa matunda, lazima ujipatiaana kwa maombi. Kuna wakati ambap mimi mwenyewe nimetaka kuandaa lakini najiupata kwamba siweze. Waklati huo huwa narudi kwa maombi.

ii. Tafakari juu ya kile ambacho unaenda kuhubiri.

iii.Anza kuandika. Ujali sana kuhusu mpangilio kwanza. Andika tu chini kile ambacho unakiwaza.

iv. Panga kazi yako kulingana na mawazo ambayo ulikuwa unakuu chini.

v. Chunguza yale ambayo ulikuwa umefanya kama:

a. Hakikisha kwamba unafahamu lengo la mwandishi. Hakikisha kwamba ujumbe wako unalenga Yesu.

b. Hakikisha katika maandalizi yako, unahakikisha kwamba unazingatia mafundisha makuu ya Biblia ambayo kifungu unafundisha kinaeleza.

c. Hakikisha ujumbe wako unaeleweka na kwamba kila mtu anaweza kufuata bila shida yoyote.

d. Hakikisha kwamba ujumbe wako unazingatia jinsi wasikilizaji wako wanapaswa kuishi kulingana na neno ambalo umelihubiri.

e. Hakikisha kwamba ujumbe wako una mhustari.

vi. Andika kila kitu chini ambacho unataka kuhubiri.

vii. Omba kuhusu unjumbe wako. Omba Mungu kwamba ujumbe huo atautumia kukubadilisha hata wewe. Mwombe Mungu azungumze kupitia wewe. Pia hakikisha kwamba utukufu ni kwa Mungu.

viii. Hubiri mahubiri yako kwa uaminifu na kwa furaha kubwa sana kwa sababu neno la Mungu.

ix. Kwa maombi wazi juu ya ujumbe ambao uliuhubiri na ujifunze kutokana na ujumbe huo.

IV Kwa kumalizia

1. Anza kuanda mahubir yako mapema sana.

2. Kumbuka kwamba inachukua muda kuandaa vyema. Usiharakishe katika maandalizi yako.

3. Kumbuka kwamba hili ni neno la Mungu ambalo unalihubiria wengine.